

Jumuiko
la
Maliasili
Tanzania



Tanzania
Natural
Resource
Forum



**Hotuba kwa DC wa Longido toka kwa wawezeshaji wa masharika ya
TNRF/CRT katika warsha ya viongozi wa mila, iliyofanyika wilaya ya
Longido tarehe 30-31/05/2007**

Utangulizi.

Mkuu wa Wilaya: Awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu za pekee na kwa niaba ya wanawarsha, kijiji cha Sinya na mashirika yalioshiriki kunda warsha hii, kwa kukubali kuja kutufungulia na kuungana nasi. Kukubali kwako mwaaliko imetudhirishia jinsi tunavyoweza kujenga mshikamano wa kusukuma mbele gurudumu la maendeleo na kuondoa umaskini kwa pamoja.

Mkuu wa Wilaya: Mafunzo haya, ni mafunzo shirikishi ya Usimamizi na Matumizi endelevu ya maliasili vijijini. Mafunzo haya yamekusudiwa ili kujenga uwezo wa jamii kupitia viongozi wa mila, watu mashuhuri hasa vijana na wakina mama ambao ni wawakilishi wa mikutano mikuu ya watu katika vijiji vyao.

Mkuu wa Wilaya: Tunatambua kuwa jamii kwa ujumla wanapaswa kufunzwa na kufahamu jinsi gani ya kuondoa umaskini kwa kuendeleza na kutumia maliasili katika vijiji vyao. Mafunzo haya ya leo itakua chachu kwa jamii kwa ujumla na pia kwa mashirika binafsi na Halmashauri ya wilaya, kubuni mbinu mbalimbali ya kutoa elimu kwa jamii kupitia mikutano mikuu ya vijiji, ili kufanikisha ufahamu wa wanachi wote jinsi ya kushiriki katika kuondoa umaskini na kuendeleza maliasili.

Mkuu wa Wilaya: Mipango shirikishi ya usimamizi na matumizi endelevu ya maliasili unaowezeshwa na mashirika ya Ujamaa –CRT, Sandy County Foundation na Jumuiko la

Maliasili Tanzania (Tanzania Natural Resource Forum) kwa ushirikiano na Mashirika mengine kama PINGOs yana malengo yafuatayo:-

- Kujenga uwezo wa jamii vijijini, ili waweze kufahamu, kuendeleza na kutumia maliasili kwa njia endelevu.
- Kuwezesha mipango na mikakati shirikishi ya usimamizi na matumizi endelevu ya maliasili na kuondoa umaskini vijijini; kama vile sheria ndogo za vijiji, mipango ya matumizi bora ya ardhi na maliasili, upimaji wa athari ya mazingira (EIA), upimaji wa ardhi ya vijiji, kupata ramani na vyeti vya ardhi ya vijiji, mikataba shirikishi, kuunda kamati za usimamizi wa mipango ya maendeleo kijijini na kuwezesha majadiliano baina ya wadau mbalimbali.
- Kubuni miradi shirikishi ya maendeleo itakayowawezesha jamii kutambua umuhimu wa kutunza na kutumia maliasili zao.
- Kufanya utafiti na ushawishi juu ya mipango ya kiseru na kisheria zinazosimamia maliasili, ili kuweza kutoa fursa sahihi kwa jamii katika ngazi ya vijiji kusimamia na kutumia maliasili kuondoa umaskini.
- Kujenga mtandao shirikishi wa majadiliano ya wadau wa maliasili vijijini ili kufanishika mahusiano ya ushirikiano wa wadau wote wa maliasili kama wanavijiji, Halmashauri za wilaya, makampuni ya utalii, mashirika binafsi ya maendeleo (NGOs/CBOs), Wizara husika na kamati ya Bunge ya Mazingira na kuondoa umaskini.

Mkuu wa wilaya: Suala la msingi kwetu kama wawezeshaji wa maendeleo vijijini ni ushirikishwaji wa wadau wa maendeleo katika ngazi husika. Hii itasaidia kujenga njozi shirikishi ya maendeleo, kwani kila mmoja wa wadau hao wa maliasili huchangia kuleta au kutoleta maendeleo kwa upande mwingine. Lakini pakiwepo na ushirikishwaji wa pamoja hasa wa jamii itatoa fursa kubwa kufikia maendeleo ya kweli.

Mkuu wa Wilaya: Ushirikishwaji wa pamoja tuna maana kuwa jamii (wanavijiji) kupitia vyombo vyao vya uwakilishi kama serikali za vijiji, uongozi wa mila, diwani na Mbunge waweze kushiriki kikamilifu katika kupanga mipango ya maendeleo, hasa uundaji wa sera na sheria zinazosimamia mipango ya maendeleo katika nchi. Tumeona kuwa bila ushirikishwaji juu ya uundaji wa sera na sheria, itakuwa vigumukwa wanachhi na hata

serikali kutekeleza sera au sheria hizo. Kwa mfano; imeonekana kuwa sheria ya usimamizi ya wanyama pori ya 19974 na sheria ya ardhi ya 1999; zinagongana hasa katika matumizi ya ardhi ya vijiji. Hivyo basi ni muhimu wananchi na wadau wahusika waweze kushirikishwa ili kuondoa migongano ya sera na sheria hizo.

Mkuu wa wilaya: Mwisho tunakuomba ungane nasi ili uweze kutushauri ni jinsi gani ya kuimarisha dhana ya usimamizi na matumizi endelevu ya maliasili na kuondoa katika ngazi za vijiji. Pia kutupa changamoto katika kuandaa mikakati na kufikia dhana ya ushirikishwaji wa kweli wa jamii ya kujiletea maendeleo yao wenyewe.

Ahsante na Karibu!